**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA FEDHA**

**BODI YA WATAALAM WA UNUNUZI NA UGAVI**

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb. Na.** AB.392/512/01/147 **Tarehe:** 27/08/2024

Wakurugenzi Wakuu wa Mashirika ya Umma,
Wakuu wa Idara Zinazojitegemea,
Watendaji Wakuu wa Mamlaka/Wakala za Serikali,
Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Majiji, Miji na Wilaya,
Wakurugenzi wa Taasisi na Mashirika Binafsi,
**TANZANIA.**

**YAH: MWALIKO WA KONGAMANO LA 15 LA WATAALAM WA UNUNUZI NA UGAVI**

Tafadhali rejea kichwa cha habari hapo juu.

2. Bodi inayo furaha kukutaarifu kuwa itakuwa mwenyeji wa Kongamano la 15 la Mwaka la Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi litakalofanyika kuanzia **tarehe 17 hadi 19 Disemba, 2024** katika ukumbi wa AICC Arusha. Kongamano hili huwaleta pamoja wadau wote wa shughuli za ununuzi na ugavi kutoka ndani na nje ya nchi ili kujadili na kubadilishana uzoefu katika masuala ya kitaalamu katika sekta ya Umma na sekta binafsi kwa kuzingatia kauli mbiu isemayo; Mabadiliko ya Mnyororo wa ununuzi na ugavi kwa usimamizi bora wa Rasilimali “(***Procurement and Supply Chain Transformation for Effective Management of Resources***)”.

3. Hivyo, Bodi inakuomba ukiwa kama mwajiri na mdau muhimu wa PSPTB kitaaluma kuwafadhili wataalam wako wa ununuzi na ugavi, wajumbe wa bodi ya zabuni na watumishi wa idara tumizi kutoka fani mbalimbali pamoja na watoa maamuzi wengine wanaohusika katika shughuli za ununuzi na ugavi ili waweze kuhudhuria kongamano hili muhimu. Kongamano hili litawasaidia kubadilishana uzoefu, maarifa na ujuzi mahsusi kwenye mnyororo mzima wa ununuzi na ugavi.

matarajio ya PSPTB kuwa kupitia Kongamano hili washiriki wataweza kuboresha utendaji kazi wao binafsi na taasisi zao ili kuleta tija katika maendeleo ya sekta binafsi na sekta ya umma. Pia, washiriki waliosajiliwa na PSPTB wataidhinishiwa **saa 24** za maendeleo ya kitaaluma (*CPD hrs*) kama hitaji lao la msingi kitaaluma.

4. Kwa wataalamu wote, usajili wa ushiriki ufanyike mtandaoni kupitia akaunti zao za usajili mtandaoni na washiriki wasio na usajili wa PSPTB, usajili wa ushiriki wao utafanyika mtandaoni kupitia; https://registration.psptb.go.tz/. Ada za ushiriki zimefafanuliwa katika jedwali hapa chini:

| Washiriki | Ada ya ushiriki |
|---|---|
| Wataalam waliosajiliwa na PSPTB | TZS.500,000/= |
| Washiriki wengine | TZS.650,000/= |
| Wanafunzi wasio na ajira | TZS.300,000/= |
| Washiriki kutoka nje ya Tanzania | TZS. 1,000,000/= |

5. Ada hizi za ushiriki ni kwa ajili ya maandalizi na uwasilishwaji wa mada, nyenzo za kongamano, kifungua kinywa na chakula cha mchana tu. Tafadhali, kumbuka kuwa hakuna washiriki watakaoruhusiwa kuhudhuria kongamano hili bila kukamilisha malipo ya ada za ushiriki zilizotajwa hapo juu. Mwisho wa kulipa ada ya ushiriki ni tarehe 30 Novemba, 2024.

6. Tunakushukuru kwa ushirikiano wako katika kujali taaluma hii adhimu ya ununuzi na ugavi kwa maendeleo ya Taifa.

7. Wasalaam,



Digitally Signed By GODFRED MBANY
Tue Aug 27 11:36:24 EAT 2024

GODFRED MBANYI
**MKURUGENZI MTENDAJI**

*GBM/pgm.*